# Maneno ya Heshima katika Kiswahili: Utendi wa Wazungumzaji Wazawa Kulingana na Rika na Jinsi zao Mjini Zanzibar

*Hassan G. Haji*

**Ikisiri**

Wazungumzaji wazawa wa Kiswahili wa Zanzibar wana dasturi zao katika kuitana. Kabla ya jina hutanguliza neno la heshima. Hali hii hutokea kwa wakubwa na wadogo, wanaojuana na wasiojuana. Makala haya yanahusu maneno ya heshima (onorafiki) katika Kiswahili, namna yanavyotumiwa na wazungumzaji wazawa kulingana na rika na jinsi zao. Makala hasa yanazungumzia namna wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili wa Zanzibar wanavyotumia maneno ya heshima katika kuitana katika mazungumzo yao ya kila siku katika nyumba na maskani zao za mazungumzo na katika sehemu zao mbalimbali za kazi. Data ya utafiti huu imeonesha kuwa maneno ya heshima yanatumika kulingana na rika za watu. Aidha, data imeonesha kuwa wazawa wa lugha ya Kiswahili huyatumia maneno ya heshima katika kuonesha uhusiano wa kifamilia na uhusiano usiokuwa wa kifamilia ili kujenga usuhuba na heshima katika mazungumzo. Wazawa wa lugha ya Kiswahili huelimishana kuitana na kuyatumia maneno ya heshima tangu wanapokuwa wadogo kama data inavyoonesha kuwa mzazi anaweza kumwita mtoto wake *baba* au *mama*, *bibi* au *babu*, *mjomba* au *shangazi* na kadhalika.

## 1.0 Utangulizi

Utafiti huu umefanywa katika visiwa vya Zanzibar ambavyo vinapatikana katika bahari ya Hindi katika Afrika Mashariki. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Visiwa hivi viko Mashariki mwa Tanzania bara. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Zanzibar ina wakazi wapatao 1,303,568. Kiswahili ni lugha mama ya Wabantu wanaoishi Zanzibar na pwani ya Tanzania bara (NBS, 2012). Karibu wakazi wote wa Zanzibar wanazungumza lugha ya Kiswahili. Kiswahili ndiyo lugha rasmi na ya taifa tangu mwaka 1967 ilipotangazwa rasmi na Baba wa taifa hayati Mwalimu Julius K. Nyerere (Mulokozi, 2002: 1).

Katika makala haya ambayo yanazungumzia utendi wa onorafiki za kijinsi na kirika katika jamii ya Wazanzibari, awali ya yote, hatuna budi kufasili istilahi tulizotumia. Tunapozungumzia utendi tuna maana ya usemaji wa lugha, yaani utamkaji wa maneno (Massamba, 2004:111), ambapo katika makala haya tunajikita kwa wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili mjini Zanzibar. Jinsi tunamaanisha asili ya kimaumbile,

yaani mwanamke na mwanamume (BAKIZA, 2010: 133), na rika tunamaanisha umri mkubwa, umri mdogo au umri unaolingana. Onorafiki ni neno tulilolitohoa kutoka lugha ya Kiingereza 'honorifics'. Kamusi ya Macmillan (2012) inaeleza maana ya neno onorafiki kuwa ni cheo anachopewa mtu kama njia rasmi ya kuonesha heshima kutokana na cheo au dhamana aliyonayo. Naye Mathews (1997) kwa upande wake, anafasili onorafiki kuwa ni kiwakilishi au kitenzi ambacho hutumiwa katika kuelezea heshima kwa mtu fulani, mfano wa hadhi kubwa. Kwa upande wao, Richards na wenzie (1985) wanaeleza kuwa onorafiki ni fomula ya upole na adabu katika lugha mahususi, ambayo inaweza kuwa viambishi maalumu, maneno au sentensi.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hao, ni wazi kuwa maneno ya heshima hutumiwa na wazungumzaji wa lugha kwa lengo la kuonesha na kudumisha heshima na upole miongoni mwa wanajamii wa lugha inayohusika. Kwa kuwa lengo lake ni hilo, basi onorafiki inaweza kutumiwa hata kama anayekusudiwa hayupo katika mazingira ya mazungumzo ili kuoneshwa upole au kupewa heshima (Habwe, 2010: 129). Kwa mfano mtu anaweza kusema:

***Mama*** Mwajuma anakwita.

Neno 'mama' kwa mfano, katika sentensi hii linaweza kutumika hata kama huyo 'Mwajuma' hayupo katika mazungumzo; alimradi yeye ni mwanamke anatajwa kwa kutanguliza neno hilo la 'mama' kwa sababu ya kumheshimu.

Makala haya yanazungumzia maneno ya heshima ya Kiswahili juu ya utendi wa wazungumzaji wazawa kulingana na jinsi na rika zao. Tumejaribu kuangalia namna wazungumzaji wazawa wakubwa, wadogo na watu wenye rika moja wanavyoitana na kutumia maneno ya heshima katika shughuli zao za kila siku. Maeneo yaliyochunguzwa ni kama vile katika nyumba zao, katika masikani zao na sehemu nyingine kama kazini na katika vyombo vya usafiri. Wazanzibari walio wengi huitana ama kwa kutanguliza neno la heshima kabla ya jina la anayeitwa au anayetajwa katika mazungumzo, mfano:

Mzu (mzungumzaji): ***Baba*** *Ali!*

Msi (Msikilizaji): Naam!

Au bila ya jina, yaani mtu anaweza kuitwa bila ya kutaja jina lake (kwa kutumia neno la heshima tu) mfano:

Mzu: ***Kaka!***

Msi: Naam!

Mzu: ***Babu*** shikamoo.

Msi: Marahaba **babu**.

Wazungumzaji wazawa wa Kiswahili wa Zanzibar huelimishana namna ya kuitana na kuyatumia maneno ya heshima tangu wanapokuwa wadogo sana. Tangu mtoto hajaweza kusema anaanza kuyasikia maneno ya heshima kutoka kwa wakubwa wake kama baba, mama, kaka au bibi kwa wao wenyewe kuitwa kwa kutumia maneno hayo ya heshima. Hii ina maana kuwa watoto hurithishwa mila hii tangu wakiwa wadogo. Inachukuliwa kuwa si heshima kwa mtoto kumtaja jina (bila ya kutanguliza neno la heshima) mtu mzima, aliyemzidi umri. Kiheshima na adabu, kabla ya jina hutangulia neno la heshima au neno la heshima peke yake bila ya jina kama ***kaka*** *Juma*! au ***kaka***! Hata hivyo, hatukupata kusikia mtoto anamwita baba yake mzazi kwa kutanguliza neno la heshima kisha jina la baba mfano, *baba* ***Hassan***! Isipokuwa baba anaweza kumwita mtoto wake kwa kutanguliza neno la heshima kisha jina la huyo mtoto kama, **Njoo** ***baba Makame*** au bila ya jina la mtoto kama: **Njoo** ***baba*** au **Njoo** ***baba angu***. Hii inatokana na sababu ya kiutamaduni au pia inachukuliwa kama dasturi au mazoea.

Maneno haya ya heshima kulingana na jinsi au rika za watu ni aina moja tu katika maneno ya heshima yanayotumika kuonesha heshima na adabu miongoni mwa Waswahili wa Zanzibar. Habwe (2010) anaeleza kuwa katika Kiswahili, onorafiki za kijinsi, ambazo yeye anaziita za kifamilia, zinaweza kutumiwa pia nje ya muktadha wa kifamilia na hadhi yake ikawa katika kuonesha upole na heshima tu miongoni mwa wazungumzaji, wala si kwa lengo la kuonesha uhusiano wa kifamilia. Hali kama hii pia inajitokeza katika mazungumzo ya wazawa wa Kiswahili wa Zanzibar. Kwa upande wao, Yoshida na Sukarai (2005: 197) wanadai kuwa katika masomo ya jadi ya Kijapani, wasomi wanadai kuwa onorafiki mtendwa (addressee honorifics) huelezea tafauti za mzungumzaji kwa mzungumzwa. Pia huonesha baadhi ya dhana za kimiktadha kama vile uhusiano hasa kati ya msemaji na msemwaji (Toujimura, 1967; Watanabe, 1971; Ide, 1982).

## 2.0 Mbinu za Utafiti

Katika kukusanya data za utafiti huu uliofanywa Wilaya ya Magharibi, Zanzibar, kutoka Januari hadi Machi, 2013 tulitumia mbinu ya dodoso na umakinifu (ushuhudiaji). Tulitumia Dodoso la Kazi ya Kukamilisha Mazungumzo (DKKM[1]) ambapo watafitiwa thelathini na tano (35) walipewa dodoso na kuzijaza. DKKM ni aina ya dodoso

[1] Mbinu hii kwa Kiingereza inaitwa *Discourse Completion Tasks/tests* (DCTs), hutumika zaidi katika ukusanyaji wa data za kipragmatiki.

linalotumika katika ukusanyaji wa data za kipragimatiki ambapo mtafitiwa hutakiwa kukamilisha maelezo/mazungumzo aliyopewa (taz. Kiambatisho A, mwishoni mwa makala haya). Mbinu hii ya DKKM inafaa sana katika kukusanyia data nyingi, kupima na kuonesha umahiri na utendi wa kipragimatiki wa wazungumzaji lugha kwa ufanisi na haraka (Aziz, 2012). Hivyo basi mbinu hii imetuwezesha kubaini namna wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili wa Zanzibar wanavyoitana kwa kutumia maneno ya heshima kwa mujibu wa jinsi na rika zao. Mbinu ya pili, kama tulivyodokeza hapo juu ni umakinifu (kwa Kiingereza observation) ambayo wengine huiita ushuhudiaji. Umakinifu ni mbinu ya kukusanyia data ambapo mtafiti anaangalia, anasikiliza na kunukuu/kurikodi data kwa umakini mkubwa. Mbinu hii ilitumika ili kusikiliza na kuandika mazungumzo ya watu mbalimbali katika mitaa na katika vyombo vya usafiri (daladala). Mbinu hii imetuwezesha kupata data halisi, asili na kwa ufanisi kutoka kwa wazungumzaji wazawa wa lugha hii ya Kiswahili kutoka Zanzibar.

## 3.0 Uwasilishaji wa Data

Uwasilishaji wa data za utafiti wetu utazingatia mbinu au zana ambazo tulitumia katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Uwasilishaji huo ni kama ifuatavyo:

### 3.1 Data za Dodoso la Kazi ya Kukamilisha Mazungumzo

Data zilizopatikana kwa kupitia njia hii ya Kazi ya Kukamilisha Mazungumzo (KKM) zinatokana na mazingira manane ambayo ni i, iii, iv, v, vi, vii, viii, na ix (taz. Kiambatanisho B) waliyopewa watafitiwa 35 ambao walikuwa ni wanafunzi wa shahada ya kwanza ya sanaa na ualimu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Wanafunzi wote walikamilisha na kurejesha madodoso yote waliyopewa na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo (kwa asilimia):

**Jedwali 1**: Maneno ya heshima yaliyokusanywa kwa kutumia DKKM

| **Mazingira** | **baba** | **mama** | **bibi** | **babu** | **kaka** | **dada** | **bwana** | **mume** | **shangazi** | **chachi** | **haloo** | **ami** | **mkwe** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **94** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 3 | 0 | 0 | 0 | **5.7** | **2.8** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2.8** | **0** |
| 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **31** | **68.5** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6 | 0 | 0 | **11** | **17** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7 | 0 | **37** | **42.8** | 0 | 0 | **2.8** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **5.7** |
| 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | **37** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **82** | **2.8** | **2.8** | 0 | |
| **Jumla** | **94** | **37** | **53.8** | **22.7** | **39.8** | **2.8** | **31** | **68.5** | **82** | **2.8** | **2.8** | **2.8** | **5.7** |

**Chanzo:** Mtafiti, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (2013)

Maneno yaliyomo katika jedwali hili ndiyo yaliyokusanywa kwa kutumia DKKM ambapo watafitiwa walitakiwa kukamilisha mazungumzo yaliyomo katika mazingira kumi[2] lakini mazingira mawili[3] yalikuwa hayahusiani na maneno ya heshima. Katika mazingira ya kwanza watafitiwa thelathini na tatu (sawa na 94%) kati ya thelathini na tano walikamilisha mazungumzo kwa kujaza neno **'baba'** ambapo wawili (sawa na 6%) hawakujaza neno lolote. Katika mazingira ya tatu, watafitiwa wawili walijaza neno **'babu'** (sawa na 5.7%); mtafitiwa mmoja alikamilisha kwa kujaza neno **'ami'** (sawa na 2.8%) na mmoja alijaza neno '**kaka'** (sawa na 2.8%). Watafitiwa ishirini na nne kati ya thelathini na tano walikamilisha kwa kujaza neno '**mume**' (sawa na 68 %.) na kumi na mmoja (sawa na 31%) walijaza neno '**bwana**' katika mazingira ya nne. Katika mazingira ya tano, hakuna mtafitiwa aliyekamilisha mazungumzo kwa kujaza neno la heshima linaloonesha jinsi ya mtu. Lakini katika mazingira ya sita, watafitiwa wanne (sawa na 11%) walijaza neno '**bibi**' na sita (sawa na 17%) walikamilisha mazungumzo kwa kujaza neno '**babu**'.

Katika mazingira ya saba, watafitiwa walijaza maneno ya heshima tofauti tofauti kama ifuatavyo: watafitiwa kumi na tatu (sawa na 37%) walijaza neno '**mama'**, watafitiwa kumi na tano (sawa na 42.8%) walikamilisha mazungumzo kwa kujaza neno **'bibi'**, watafitiwa wawili (sawa na 5.7%) walikamilisha kwa kujaza neno **'mkwe**', mmoja (sawa na 2.8%) alijaza neno '**dada**' na watatu (sawa na 8.5%) hawakujaza neno lolote. Katika mazingira ya nane, watafitiwa kumi na tatu (sawa na 37%) walikamilisha kwa kujaza neno **'kaka'** ambapo watafitiwa ishirini na mbili (sawa na 62.8%) hawakujaza neno lolote. Hatimaye katika mazingira ya tisa, watafitiwa ishirini na tisa kati ya thelathini na tano (sawa na 82%) walikamilisha kwa kujaza neno '**shangazi**', mtafitiwa mmoja (sawa na 2.8%) alijaza neno '**chachi**' (shangazi) na mmoja (sawa na 2.8) alijaza neno '**haloo**' (mama mdogo).

### 3.2 Data za Umakinifu

Katika utafiti huu, mbinu ya umakinifu pia ilitumika kukusanyia data. Kwa kutumia mbinu hii data ilikusanywa katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar ambayo ni nyumbani na kwenye daladala (vyombo vya usafiri). Data hizo zilikuwa kama ifuatavyo:

---

[2] Mazingira 'situations' ni mazungumzo katika DKKM katika miktadha mbalimbali (taz. Kiambatisho A na B kuna mazungumzo 1-10).
[3] Taz. Kiambatisho mazingira 2 na 10.

**Jedwali 2:** Maneno ya Heshima Yaliyokusanywa katika Mazungumzo ya Nyumbani

| Mazungumzo | Maneno ya Heshima | Mazungumzo | Maneno ya Heshima |
|---|---|---|---|
| i. | Bibi | vii. | Da (dada) |
| ii. | Ba (baba) | viii. | Ka (kaka) |
| iii. | Bi (bibi), dada | ix. | Mama |
| iv. | Baba | x. | Dada |
| v. | Ma (mama) | xi. | Dada |
| vi. | Babu | xii. | mkuu (baba mkuu) |

**Chanzo:** Mtafiti, Mjini Zanzibar (2013)

**Jedwali 3:** Maneno ya Heshima Yaliyokusanywa katika Mazungumzo ya kwenye Daladala

| Mazungumzo | Maneno ya Heshima | Mazungumzo | Maneno ya Heshima |
|---|---|---|---|
| i. | Dada | vi. | Kaka |
| ii. | Ami | vii. | Baba |
| iii. | Kaka | viii. | Anko |
| iv. | Bwana | ix. | Anti |
| v. | Ami | x. | Faza |

**Chanzo:** Mtafiti, Mjini Zanzibar (2013)

## 4.0 Uchambuzi wa Data na Maelezo

Kama tulivyosema kutoka mwanzo kuwa makala yanachunguza namna wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili wa mjini Zanzibar wanavyotumia maneno ya heshima katika kuitana katika mazungumzo yao ya kila siku kulingana na jinsi na rika zao. Sehemu hii inachambua data hizo. Ingawa mjadala hapa chini unaonekana kulenga rika zao lakini kimsingi katika kukijadili kipengele hiki kipengele cha jinsi (mwanamke na mwanamume) pia kinajibainisha:

### 4.1 Utendi wa Wazungumzaji Wazawa wenye Umri Mdogo

Kwa jumla, data za utafiti huu zinaonesha kuwa wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili wa Zanzibar wenye umri mdogo hutumia maneno ya heshima katika kuwaita watu wanaowazidi umri kulingana na jinsi zao kama sehemu ya utamaduni wao. Maneno kama *baba, babu, kaka, ami,* na *baba mkuu* hutumiwa na wenye umri mdogo kuwaita watu wanaowazidi umri. Watu hawa wazima huweza kuwa wana uhusiano nao kifamilia, wanaojuana tu au wasiowajua kabisa ili kuonesha heshima, adabu au upole katika mazungumzo. Tukirejelea data za utafiti wetu katika KKM katika mazingira ya kwanza tunaona kuwa mtoto alimwita mzazi wake wa kiume, 'baba'. Hii inaonesha kuwa mtoto wa Kiswahili anapozungumza na baba yake hutanguliza neno la heshima:

'*baba* shikamoo'. Aidha, hali hii imejitokeza katika mazungumzo ya nyumbani na katika daladala; mfano katika mazungumzo haya ya nyumbani:

> **Msichana:** *Baba*, pesa za juzuu.
> **Baba**: Haya, nishasikia.

Kwa mujibu wa utamaduni wa jamii hii mtoto hana budi kuita hivyo ili kuonesha heshima zaidi. Katika jamii nyingine inawezekana mtoto akamwita baba bila ya kutanguliza neno "baba', kwa mfano, hutumia jina la huyo baba tu, mfano: John n.k.

Katika mazungumzo yafuatayo yaliyofanyika katika daladala, utingo alitumia neno la heshima, 'baba' katika kuonesha upole na heshima kama hivi:

> **Utingo**: Usiwe mkali *baba*, sogea kidogo.
> **Abiria**: Sio ukali. Nafasi hamna.

Data pia zinabainisha kuwa wazungumzaji wazawa wenye umri mdogo wana desturi ya kuwaita wazazi wao wa kiume na kike kwa maneno ya heshima, *baba* au *mama* kabla ya kuanza mazungumzo yao kama ilivyojitokeza katika mazingira ya (i) katika Kiambatisho A ambapo watafitiwa 33 kati ya 35 walijaza neno *baba.* Hali hii inadhihirisha kuwa Waswahili hawawezi kuwaita wazazi wao bila ya kutanguliza neno la heshima.

### 4.2 Utendi wa Wazungumzaji Wazawa, Watu Wazima

Utafiti huu unaonesha kuwa wazungumzaji wazawa, watu wazima hutumia maneno ya heshima kulingana na jinsi zao kama wanavyotumia watoto wadogo kuwaita wakubwa zao ili kuonesha upendo na upole zaidi. Maneno yanayotumiwa na wakubwa ndiyo yaleyale yanayotumiwa na wenye umri mdogo. Utafiti unaonesha maneno kama *babu, bibi, baba, kaka, dada* na *mama* hutumiwa na wakubwa kuwaita wadogo. Katika mazungumzo ya kawaida nyumbani, baba au mama anaweza kumwita mtoto wake wa kiume 'baba', mtoto wake wa kike 'mama', mjukuu wa kike humwita 'bibi' na mjukuu wa kiume humwita 'babu.' Mathalani, katika Kiambatisho A katika mazingira ya 6 watafitiwa walijaza ama *bibie* au *bibi*. Hali hii hujitokeza hata kama wazungumzaji hawana uhusiano wa kifamilia, kama alivyotumia utingo katika mazungumzo yake na abiria; namba (i) alitumia neno *dada*, (ii) alitumia neno *ami* na (vii) alitumia neno *baba* (taz. Kiambatisho C). Utingo alitumia maneno haya ili kuonesha upole na upendo kwa abiria wake.

### 4.3 Utendi wa Wazungumzaji Wazawa wenye Rika Moja

Data za utafiti huu pia zinaonesha kuwa wazungumzaji wazawa wa Kiswahili wenye rika moja wanatumia maneno ya heshima kulingana na jinsi zao. Kwa vijana, maneno kama

*anko, anti, braza, kaka, dada, bwana* na wakati mwingine maneno kama *bi (bibi)*, *ustadhi* au *sheikh* hutumiwa na wazungumzaji wenye rika moja. Hali hii hutokea katika kudumisha utamaduni wa Waswahili wa kuitana kwa heshima na kuonesha upole (taz. mazungumzo kwenye daladala namba (i), (iv), (vi) na (viii)).

### 4.4 Athari za Lugha Nyingine

Katika utafiti huu tumegundua pia kuwa kuna matumizi ya maneno ya heshima ambayo yana asili ya lugha nyingine kama vile Kiarabu na Kiingereza. Kiingereza ni lugha rasmi na ya kufundishia nchini Tanzania kuanzia ngazi ya elimu ya sekondari. Kwa hivyo, wazawa wa Kiswahili wameathirika sana na lugha hii ya Kiingereza. Kihistoria Tanzania ilitawaliwa pia na Mwingereza. Ndiyo maana utingo wa daladala aliyatumia maneno kama **anko** (uncle), **anti** (aunt), **faza** (father) (taz. Kiambatisho C). Aidha, kwa upande wa matumizi ya lugha ya Kiarabu kuna maneno ya heshima kulingana na jinsi za watu kama vile **haloo** (khalat = mama mdogo), **ami** (baba mdogo/baba mkuu), **ustadhi** (mwalimu wa kiume) na **sheikh** hutumiwa sana na wazungumzaji wazawa wa lugha hii ya Kiswahili katika mazingira yasiyo rasmi. Athari hii inatokana na ukweli kwamba, Wazanzibari walio wengi ni waumini wa dini ya Kiislamu na lugha ya dini ni Kiarabu; ndiyo maana Waswahili wanayatumia maneno kama hayo (taz. Kiambatisho C).

### 4.5 Vifupisho vya Maneno ya Heshima

Utafiti huu pia umegundua kuwa mara nyingi katika mazungumzo au katika kuitana, wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili wa Zanzibar, huyasema maneno hayo kwa vifupisho. Hii ni kutokana na kwamba moja kati ya sifa za lugha ya mazungumzo ni kutumia lugha fupi au ufupisho wa maneno ili kurahisisha mazungumzo na kuyafanya yaende haraka. Mifano ifuatavyo inadhihirisha jambo hili (taz. pia Viambatisho B na C):

**Jedwali 4**: Vifupisho vya Maneno ya heshima katika mazungumzo ya nyumbani na daladala.

| Na. | Kifupisho | Neno Kamili |
|---|---|---|
| 1. | da | dada |
| 2. | ma | mama |
| 3. | bi | bibi |
| 4. | ka | kaka |
| 5. | ba | baba |

**Chanzo:** Mtafiti, Mjini Zanzibar (2013)

Mara nyingine, vifupisho hivi vinapotumiwa hufuatiwa na jina la mtu kama vile: *Bi. Sindugu, Ka Juma*, n.k. iwapo mzungumzaji ni mdogo kiumri au wote wawili wana rika moja. Ikiwa wazungumzaji wana uhusiano wa kifamilia au wa kiukoo, basi mdogo akimwita mkubwa atatumia vifupisho pamoja na jina la mtu au cheo chake katika familia. Mfano, *Ma Mnono* (Mama Mnono) au *Ba Mkuu* (Baba Mkuu). Aidha, ikiwa mtoto anamwita mzazi wake wa kike au wa kiume hapaswi kutaja jina la mzazi wake. Kwa mfano, mimi baba yangu anaitwa Gora; sisemi au simsalimii kwa kusema: "Ba (baba) Gora shikamoo". Nitasema, "Ba/baba shikamoo". Isipokuwa mtu mwingine, kuonesha heshima, anaweza kusema: "Ba/baba Gora shikamoo". Kwa mtoto kuweka jina la baba/mama si heshima, inatosha tu kusema 'baba/mama' (taz. Mazungumzo ya nyumbani namba (i), katika Kiambatisho B).

**5.0 Hitimisho**

Makala haya yamechunguza utendi wa wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili Zanzibar katika kuitana kwa kutumia maneno ya heshima kulingana na jinsi na rika zao. Tumeona jinsi wadogo wanavyowaita wakubwa, wakubwa wanavyowaita wadogo na wazungumzaji wa rika moja wanavyoitana. Kwa muhtasari, data zimeonesha kuwa maneno ya heshima ya kijinsi kama *baba, mama, kaka, dada, babu*, na *bibi* hutumiwa na watu wote, yaani wakubwa, wadogo na wenye rika moja, kutegemea uhusiano wao wa kifamilia au kuonesha upole na heshima. Halikadhalika, data za utafiti wetu zimebaini kuwa kuna maneno ya heshima kulingana na jinsi za watu, ambayo yanatokana na athari za lugha nyingine. Maneno kama *ami, sheikh, ustadhi*, na *haloo* yanatokana na lugha ya Kiarabu na maneno kama *anti, anko*, na *faza* yanatokana na lugha ya Kiingereza ambayo hutumiwa na wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kiswahili katika kuitana, kwenye mazungumzo na salamu pia. Kwa mujibu wa uchunguzi huu, maneno ya heshima ya kijinsi hutumiwa na Waswahili ndani ya familia/ukoo na nje ya familia. Juu ya hivyo, utafiti zaidi unahitajika kufanywa juu ya maneno mengine ya heshima yasiyokuwa ya kijinsi kama vile bosi, mkwe, mwalimu na mjomba.

**Marejeo**

Aziz, H. E. A. (2012). 'Assessing Pragmatic Competence through DCTs: A Response to an Everlasting Issue'. Imedurusiwa 23/12/2014 kutoka http://aminudin.staf.upi.edu/2012/02/17/assessing-pragmatic-competence-through-dcts-a- response-to-an-everlasting-issue/

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Cristal, D. (2003). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. London: Blackwell. CUP.

Habwe, J. H. (2010). "Politeness Phenomena: A Case of Kiswahili Honorifics" katika Swahili Forum Imedurusiwa 28/01/2013 kutoka http://www.qucosa.de/fileadmin/data/qocosa/documents

Macmillan (2012) katika http://www.macmillandictionary.com/dictionary/british/honorific imesomwa tarehe 29/01/2013

Massamba, D. P. D. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mathews, P. H. 1997. *A Concise Oxford Dictionary of Linguistics*. New York: OUP.

Mulokozi, M. M. (2002). "Kiswahili as a National and International Language". Imedurusiwa 29/01/2013 kutoka http://www.chakita.org/documents/kiswahili%20Mulokozi.pdf

National Bureau of Statistics (NBS). (2012). Sensa 2012: Analytical Report. Imedurusiwa 30/01/2013 kutoka http://www.nbs.go.tz/sensa2012/index.php

Sukarai, C. na Yoshida, M. 2005. "Japanese Honorifics as a Marker of Sociocultural Identity: A View from Non-Western Perspective" katika Lakoff, R. T na Ide, S. (2005). *Broadening the Horizon of Linguistic Politeness*. John Benjamins Publishing Company. Kimedurusiwa 27 /01/2013 kutoka http://www.amazon.com/gp/product/images/902725382X/ref=dp_image_0?ie=UTF8&n=283155&s=books.